# OFISI YA RAIS TAMISEMI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

SHULE YA SEKONDARI LUFINGO,

S. L. P 512,

**TUKUYU.**

Barua pepe……………………….

Mob: 0712858806

Tarehe ……………………..

**Kumb. Na. LSSS/IN/2020…………………………………**

**Jina la Mwanafunzi …………………………………………………………………………………….**

**S. L. P ……………………**

**………………………………**

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUFINGO WILAYA YA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.</u>**

**1.0. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (1) katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Lufingo ipo umbali wa Km. 16 Magharibi mwa Mji Mkuu wa Halmashauri ya wilaya ya Rungwe. Usafiri wa basi kutoka Mjini Tukuyu unapatikana katika Kituo cha mabasi cha Tukuyu. muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11 /01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18 /01/2021 ndani ya siku saba.

**2.0. MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1. Sare za Shule**

**(a)** Sare ya shule hii ni suruali rangi ya kijani jeshi moja na nyingine rangi nyekundu damu ya mzee na shati mbili nyeupe mikono mifupi kwa wavulana, na kwa wasichana ni sketi mbili, moja rangi ya kijani jeshi na nyingine nyekundu damu ya mzee. Pia mashati mawili mikono mifupi. Viatu vyeusi jozi moja[pea mbili] na soksi nyeupe wasichana na nyeusi kwa wavulana. Sare ziwe na heshima, sketi kwa wasichana zipite magoti na kwa wavulana suruali za kubana na zenye milegezo hazitakubaliwa.

**(b)** Rangi ya HIJABU ifanane na za shule.

**(c)** Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta moja rangi nyekundu, T-shirt moja rangi ya kijivu na raba za michezo kwa wavulana na wasichana.

**2.2.** Daftari (Counter Book) 12, kalamu za wino na risasi za kutosha na mkebe wa Hisabati.

**2.3.** Chakula cha wanafunzi wa kutwa gharama itaelezwa baada ya mkutano wa wazazi. Nauli ya kwenda na kurudi nyumbani pamoja na matibabu ni wajibu wa mzazi.

## 3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:

**3.1.** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla ni **JAMBO LA LAZIMA.**
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na Ratiba ya Shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia Ratiba ya shule wakati wote na…….
(i) Kutunza mali za Umma.

**3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-**

(a) Wizi
(b) Uasherati na Ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(e) Kupigana au kupiga.
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
(g) Kudharau Bendera ya Taifa.
(h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
(i) Kuoa au kuolewa.
(j) Kutoa mimba.
(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(m) Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0.** Kila mwanafunzi atatakiwa kujaza fomu zifuatazo zilizoambatanishwa na barua hii na kuwasilishwa wakati wa kuripoti

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi na Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana,

…………………………………….

**GODFREY NICODEMUS**
**MKUU WA SHULE**

## VITU VINGINE ANAVYOTAKIWA KUJA NAVYO MWANAFUNZI

1. Vifaa vya Usafi – Fagio , Jembe pamoja na ndoo ya lita kumi [mpya]
2. Truck suit ( Blue bahari yenye ufito mweupe)
3. Kamusi ya Kingereza.
4. Rula ndefu na angavu.
5. Mathematical table[four figure]

## SHULE YA SEKONDARI LUFINGO

### FOMU H.B. HABARI BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI

---

1. Jina la Mwanafunzi (jina hili ndilo litakalotumika siku zote bila kubadilika)

   …………………………………………………………………………………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………………………………….

3. Mahali alipozaliwa (Kijiji) ……………………………… Wilaya ………………………………
4. Mahali anapoishi sasa (Wilaya) ……………………… (Kata) …………………… (Kijiji)…………………...
5. Jina la Baba / Mlezi …………………………………………………………………….
6. Anuani ya Baba / Mlezi …………………………………………………………….
7. Jina la Mama / Mlezi ……………………………………………………………………..
8. Dini ya Mwanafunzi ……………………………………………………………………..
9. Dini ya Baba / Mlezi ……………………………………………………………………….
10. Dini ya Mama / Mlezi …………………………………………………………………….
11. Kazi ya Baba / Mlezi ……………………………………………………………………..
12. Michezo atakayoshiriki shuleni ni: ………………………………………………………………………......
    ……………………………………………………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………………………………………………
    …………………………………………………………………………………………………………………..
13. Shule ya Msingi aliyosoma ……………………………………………………………………………….
14. Mwaka alioanza shule ya msingi ……………………………………………………………………..
15. Mwaka anaoanza shule ya sekondari …………………………………………………………………
16. Mwaka atakaomaliza shule ya sekondari ……………………………………………………………
17. Kiapo cha mwanafunzi ………………………………………………………………………………………….
    ……………………………………………………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………………………………………………

**Saini ya Mwanafunzi ……………………………………………………………………………**

**SAINI YA MKUU WA SHULE: ………………………………………………………………**

# UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI

**NB:** Fomu hii ijazwe na mzazi/ mlezi katika sehemu yake pamoja na mwanafunzi katika sehemu yake kisha irudishwe shuleni.

Mimi ………………………………………………………….. mzazi / mlezi wa ………………………………………………

nimeelewa na ninakubali masharti yote yanayohusu mtoto wangu kuingia shule ya Sekondari

Lufingo. Nitampatia mahitaji yote yanayotakiwa na nitashirikiana na walimu wa shule ya Sekondari Lufingo katika kumlea mtoto wangu ili apate kunufaika na elimu atakayoipata shuleni.

**Saini ya mzazi / mlezi** …………………………………

Mimi ……………………………………………………………………………………….ambaye ni Mwanafunzi niliye chaguliwa kujiunga na shule hii, naelewa kuwa ni dhamana kubwa kwangu kupata nafasi katika shule ya serikali, naahidi kutii sheria ya shule na nitajitahidi kuwa mwanafunzi mwema na mwenye bidii, nidhamu darasani na katika kazi zote za mikono kwa muda wote nitakaosoma katika shule hii. Sitashiriki katika vikundi viovu, migomo au maasi ya aina yoyote. Naahidi daima nitaweka moyo wa kizalendo mbele, utovu wa nidhamu kwangu itakuwa mwiko.

**Saini ya mwanafunzi** ……………………………….

Tarehe ……………………………………

## FORM (REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION) THIS FORM IS TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER

Name of Pupil ……………………………………………………………………………………….

Age ……………………………………………… Sex ………………………………………………..

The above named has been examined is respect of:-

(a) STOOL ……………………………………………………………………………………………………………………..

(b) URINE ……………………………………………………………………………………………………………………

(c) CHEST ……………………………………………………………………………………………………………………

(d) BLOOD …………………………………………………………………………………………………

(e) EYES ………………………………………………………………………………………………………………………

(f) EARS ……………………………………………………………………………………………………

(g) OTHER FINDINGS …………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………

I am satisfied that the above named pupil is fit / not fit to pursue further studies in a Secondary school.

……………………………………..                                                  …………………………………

**SIGNATURE**                                                  **DATE**

**……………………………………..**                                                  **…………………………………**

**DESIGNATION**                                                  **STATION**